

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
10 Mei 2008**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe  
Ally Saidi Mwishehe  
Aseli Wilison  
Edgar R Paulo  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Husein Hamza Hamisi  
Juma Ali Salehe Jongo  
Jumanne Idd Selemani  
Kassim Bakari  
Markus Weise  
Mussa Omari  
Saidi Mbaruku

**Mradi wa Usalama Barabarani - Wamba Memorial Fund**

Siku ya jumanne, Juma, Elaine na Markus walikutana na wakilishi wa Chuo cha Usafirishaji na wakilishi wa HUWATA kwenye ofisi ya Chuo cha Usafirishaji. Wapo tayari kushirikiana nasi katika mradi huu, na kutupa darasa na uwanja kwa ajili ya “training of trainers”. Walipendekeza tualike mwakilishi wa traffic police kwenye training of trainers pia. Tulikubali kwamba kila shirika litatoa nakala za mipango ya mafunzo ambayo wanayo kwa mashirika mengine kwa email. Pia tulikubali kwamba Markus na Juma watakutana na HUWATA tena siku la jumanne kuongea zaidi kuhusu shule gani kuzichagua.

Elaine alitumia email kwa Wamba Memorial Fund na walijibu kusema kwamba hela haikuenda vizuri moja kwa moja na wataomba benki kutumia kwa kupitia benki ya kati kati.

Tuliongea kuhusu suala la shule. Tulikubali kwamba tutatembelea Mbondole Secondary School jumamosi tarehe 24 Mei na tutaondoka ofisini saa moja asubuhi. Tulikadiri itaweza kuchukua masaa matatu kufika kule. Tutatembea na vifaa vya ufundi, chakula na maji ya kunywa ya kutosha. Pia tutatoa posho ndogo kwa sababu washiriki watakosa siku nzima ya kazi.

Edgar alipendekeza tushirikiana na shule moja ya Tungi, Kigamboni kwa sababu kuna wapanda baisikeli wengi kule na alisema atapata namba za simu zao. Ali Athman alipendekeze kila mwanachama aongee na marafiki yake kupata mawazo ya shule gani ina wanafunzi wanaoenda shuleni na baisikeli, hasa wilaya ya Kinondoni. Pia tulikuwa na wazo kuwasiliana na Kali Mata kupata contacts za shule ambazo zipo Kigamboni.

**Redio**

Mejah alitumia message kusema kwamba aliwasiliana na Radio One kipindi cha mazingira na wameshatayarisha ratiba yao ya mwezi huu lakini wataweza kutupa nafasi mwezi ujao. Mejah ataendelea kufuatalia.

**Mambo ya hela**

Juma alipokea Tsh 20,000 kabla ya mkutano na Tsh 7,000 wakati wa mkutano za hela za guta kwa wiki nne. Alimpa Jumanne Tsh 10,000 kwa ajili ya lino. Alitumia Tsh 2,000 kupata nakala ya ufunguo wa sanduka la posta. Sasa ana Tsh 29,000 ya hela ya UWABA nyumbani.

**Traffic police**

Elaine alimpigia simu Bwana Balele na alisema tumtembelee tena kuamua siku ya mkutano. Juma na Markus wataenda kule jumanne na watajaribu kupata mkutano alhamisi kwa ajili ya wanachama wa UWABA.

**Helmeti**

Juma alisema kwamba kuna helmeti tatu zinazobaki kutoka kwa uzinduzi, na Mejah atatupa helmeti tano. Hata hivi hatuna uhakika kama kuna helmeti ndogo kwa ajili ya Mussa Alex – kama hakuna basi tupate helmeti ndogo sokoni.

**Mambo mengine**

Wanachama walipendekeza kwamba picha za uzinduzi ziwepo ofisini. Ali Athman alipendekeza tupate ramani ya mkoa wa Dar es Salaam kuweka ofisini na atatafuta taarifa ya bei na zinapatikana wapi. Wanachama walimkumbusha Elaine atayarishe vitambulisho.